



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA WAJANE DUNIANI, 2026

Dodoma, 18 Juni, 2026.

Ndugu Wanahabari; napenda kutoa taarifa kuhusu Siku ya Kimataifa ya Wajane Duniani tarehe 23 Juni ambapo, kila mwaka nchi yetu huungana na Jumuiya ya Kimataifa kuadhimisha. Mwaka huu kaulimbiu ni “Imarisha Haki, Utu na Uwezeshaji Kiuchumi kwa Wajane” na maadhimisho yatafanyika kila mkoa. Aidha, maadhimisho haya yanatoa fursa ya kutambua mchango wa wajane katika maendeleo ya familia, jamii na Taifa, kutathmini changamoto zinazowakabili pamoja na kuimarisha hatua za kuhakikisha wanapata haki, heshima na fursa za maendeleo.

Ndugu Wanahabari; Siku ya Wajane Duniani iliasisiwa na Bw. Lord Raj Loomba aliyeanzisha Kampeni za kutetea Haki za Wajane baada ya kushuhudia changamoto alizokumbana nazo mama yake alipobaki mjane akiwa na umri mdogo. Juhudi hizo zilipelekea Umoja wa Mataifa kupitia Azimio Na. A/RES/65/189 la tarehe 21 Desemba, 2010 kutambua rasmi tarehe 23 Juni ya kila mwaka kuwa Siku ya Kimataifa ya Wajane.

Ndugu Wanahabari; kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa, duniani kuna zaidi ya wajane milioni 258 ambapo takribani milioni 115 wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo umaskini, unyanyasaji, ukatili, kunyimwa haki za urithi na kutengwa na jamii. Nchini Tanzania, matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 yanaonesha kuwa idadi ya wajane ni 1,396,262 sawa na 4.4% ya wanawake wote nchini.

Ndugu Wanahabari; licha ya mchango mkubwa wa wajane katika malezi ya familia na maendeleo ya jamii, wengi bado wananyimwa haki za kumiliki na kurithi mali, wanafukuzwa katika makazi yao, wananyanyaswa na kutengwa kijamii, wanakosa fursa za kiuchumi na wanashindwa kupata msaada wa kisheria wanapodai haki zao. Hali hii inasisitiza umuhimu wa kuendelea kuchukua hatua madhubuti za kuwalinda na kuwawezesha wajane katika nyanja zote za maendeleo. Hivyo, maadhimisho ya mwaka huu yanaendelea kulenga kuhamasisha jamii, Serikali na wadau mbalimbali kuhakikisha wajane wanapewa heshima ya utu wao sambamba na haki zao na hawanyanyaswi na yeyote. Vilevile, maadhimisho yatajielekeza kwenye kusisitiza umuhimu wa kuwawezesha wajane kiuchumi kupitia upatikanaji wa mikopo, mafunzo ya ujasiriamali, ajira na fursa mbalimbali za uzalishaji mali ili waweze kujitegemea na kuchangia maendeleo ya taifa.

Ndugu Wanahabari; kuelekea utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Serikali inatambua kuwa, maendeleo jumuishi hayawezi kufikiwa ikiwa makundi maalum wakiwemo wajane, yataendelea kubaki nyuma kiuchumi na kijamii. Hivyo, uwezesaji wa wajane ni sehemu muhimu ya uwekezaji katika mtaji wa watu, kupunguza umaskini, kuimarisha usawa wa kijinsia na kujenga uchumi shirikishi unaowanufaisha wananchi wote. Aidha, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inasisitiza ushiriki sawa wa wanawake katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, jambo ambalo linakwenda sambamba na dhamira ya kuwawezesha wajane kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji na uongozi.

Ndugu Wanahabari; kuelekea kilele cha maadhimisho haya, wizara itaendelea kuratibu vipindi vya elimu kwa umma ili jamii ifahamu juu ya changamoto za wajane na jinsi gani Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuchukua hatua ili wajane wengi zaidi wasibaki wanyonge bali wachukue hatua stahiki kwa wakati.

Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwaratibu viongozi wengine wote wa kijamii wakiwemo viongozi wa dini, mila, mashirika ya kiraia, sekta binafsi, vyombo vya habari, watu maarufu na wananchi kwa ujumla kuweka mkazo katika kulinda haki za wajane, kupinga vitendo vya ukatili na unyanyasaji pamoja na kuwawezesha kiuchumi. Pongezi ziende kwa Vyama mbalimbali vya Wajane kikiwemo CCWWT, TAWIA, Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa kuendelea bila kuchoka kila mmoja kwa nafasi yake kuwaratibu Wajane na kutekeleza afua za kuendeleza.

Ndugu Wananchi, ninawatakia Wananchi wote, ufuatiliaji mwema wa elimu kwa umma kuelekea kilele cha siku ya Wajane duniani tarehe 23 Juni, 2026.



Dkt. Dorothy Gwajima

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

